# Nifanye nini ili kujua kama nina au sina maambukizi ya Virusi vya UKIMWI?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ipo njia moja ya kuhakikisha kama umeambukizwa Virusi vya UKIMWI na UKIMWI au hapana. Njia hii ni ya kupima damu yako katika vituo vyenye utaalamu wa upimaji. Ni muhimu kukumbuka kuwa Virusi vya UKIMWI, vinaonekana kwenye damu ya binadamu miezi mitatu baada ya kuambukizwa. Kipindi hiki kati ya kuambukizwa hadi kufikia miezi mitatu kipimo hiki i hakiwezi kuonyesha kama maambukizi ya virusi yapo au hayapo. Kipindi hiki ni cha hatari sana , kwani aliyeambukizwa anaweza kuwaambukiza wengine bila kujua.